# JARIBIO LA MTIHANI
# DARASA LA NANE -2022

002

## KISWAHILI:
## LUGHA

**Muda: Saa 1 Dak. 40**

## NYERI COUNTY

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lionyeshe katika **KARATASI YA MA JIBU** na wala sio katika kijitabu cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu: -

   **NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye nambari zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **Mfano:**

   **Katika kijitabu cha maswali:**

15. Jina jingine la shangazi ni?
   A. Hale
   B. Halati
   C. Umbu
   D. Amalati

   Jibu sahihi ni **A.**

   **Katika karatasi ya majibu**

   15. ~~[A]~~ [B] [C] [D] 17. [A] [B] [C] [D] 18. [A] [B] [C] [D] 19. [A] [B] [C] [D]

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 15, kisanduku chenye herufi A ndicho kilichochorwa kistari.
11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.

FUNGUA KURASA

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Jaza vihasho kwa jibu mwafaka ili kukamilisha kifungu***

Kunyambua vitenzi ni___1___vitenzi katika___2___mbalimbali kwa kuvigeuza kwenye kiishio au ukipenda ___3___.

Vitenzi___4___ ___5___au hubadilika mahali ___6___mzizi wa kitenzi ___7___. Kamusi husaidia sana kukupa mzizi___8___ kitenzi . Kwa mfano , kitenzi kataa kwenye kamusi___9___ kata. a. Naam, vitenzi hunyambuliwa katika kauli mbalimbali kama vile kufanya, kufanyika , kufanyana , ___10___ kufanyiwa, kufanyia kando na kauli nyinginezo

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. kuvibadili | B. kuyabadili | C. kuvichagua | D. kuviweka |
| 2. | A. maumbo | B. sampuli | C. mseto | D. kauli |
| 3. | A. ngeli anuwai | B. kiambishi tamati | C. kiambishi ngeli | D. kiambishi awali |
| 4. | A. lingine | B. mwingine | C. vingine | D. zingine |
| 5. | A. hunyambulika | B. hunyambulisha | C. hunyambuliwa | D. hunyambulishwa |
| 6. | A. zenye | B. kwenye | C. mwenye | D. penye |
| 7. | A. hii | B. hicho | C. hilo | D. hiki |
| 8. | A. ya | B. za | C. wa | D. mwa |
| 9. | A. kingeandikwa | B. vitaandikwa | C. litaandikwa | D. kitaandikwa |
| 10. | A. kufanyua | B. kufanyiliwa | C. kufanyizia | D. kufanyikia |

Hakika___11___chamboni mwa siasa . Hata hivyo katika___12___ huu wa siasa umewahi kuketi ___13___ na kujiuliza siasa hasa ni nini ? Kila baada ya nusu ___14___ watu wengi huzuka wakitaka kuchaguliwa kaunti, kuwakilisha ___15___ au hata kuwania kiti kikuu cha urais au ukipenda nyadhifa ya urais.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. | A. tuko | B. tumo | C. tupo | D. tulipo |
| 12. | A. muhula | B. mfumo | C. msimu | D. kipindi |
| 13. | A. ukaenzi | B. ukaota | C. ukatafakari | D. ukapanga |
| 14. | A. msimu | B. mwaka | C. karne | D. mwongo |
| 15. | A. eneo bunge | B. kata ndogo | C. taifa | D. wilaya |

**Chagua jibu sahihi kutoka nambari ya 16-30**

16. **Andika umoja wa sentensi ifuatayo :**
Nyusi huwa mapajini pa nyuso za wanadamu
A. Usi huwa pajini pa uso wa mwanadamu
B. Unyusi huwa pajini pa uso wa mwanadamu
C. Unyusi huwa pajini pa unyuso wa mwanadamu
D. Usi huwa pajini pa unyuso wa mwanadamu

17. Kijiti kikavu kilivunjika __________ na kuanguka chini __________
A. kacha, ta　　B. twa/ pu
C. pwa/ chubwi　　D. kacha/ mwa

18. **Badilisha vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendesha :**
Oa, kaa, jua
A. Olea, katika, juza
B. Oza, kalisha, juvya
C. Olesha, ketisha, juvya
D. Oesha, ketisha, julisha

19. Panga maneno yafuatayo ili yawe na mfululizo ufaao
A. Mtondogoo, mtondo, keshokutwa, kesho , leo, jana, juzi
B. Keshokutwa, mtondo , mtondogoo, kesho, leo, jana, uzi
C. Mtondogoo, juzi, kesho, jana, mtondo, leo, kesho kutwa
D. Mtondo, mtondogoo, juzi, jana, kesho kutwa, kesho, leo

20. **Geuza sentensi ifuatayo katika hali ya udogo**
Ndizi zilizoiva zote zipewe watoto
A. Madizi yaliyoiva yote yapewe matoto
B. Kidizi kilichoiva chote kipewe kitoto
C. Dizi lilioiva lote lipewe toto
D. Vidizi vilivyoiva vyote vipewe vitoto

21. Mtwana amempelekea bibi jimbi. Kinyume chake ni_______
A. Mtwana hajampelekea bibi jimbi
B. Mjakazi amemrudishia babu koo
C. Mjakazi amempelekea bwana koo
D. Bwana amemrudishia bibi jimbi

22. Ni mapambo yapi yaliyoambatanishwa vyema na yanapovaliwa ?
A. Bangili, kikuku, kikuba - mkono
B. Mkufu, jaribosi, kidani - shingo
C. Kipini, kikero, hazama - pua
D. Herini, kipuli, utunda - sikio

23. Chagua sentensi iliyo sahihi kisarufi
A. Katika sokoni, maembe yamejaa nomi
B. Tafadhali niwekee pesa hizo kwa kibeti changu
C. Niliskia habari za kufaulu kwake katika redio
D. Naelekea kwenye uwanja kutazama kandanda

24. Chagua sentensi yenye kiambishi tamati rejeshi
A. Ukianguka hapa utaumia
B. Msichana apendaye kazi ni huyu
C. Wasichana wanaoimba watatuzwa
D. Kitabu kinachouzwa ni cha hadithi

25. Neno lipi ambalo si kitawe kati ya haya ?
A. Kaa　　B. Paka
C. Kopa　　D. Sahibu

26. **Chagua <u>kivumishi</u> na <u>kielezi</u> katika sentensi hii :**
Nguo iliyofuliwa na yaya yule imeng'aa kabisa
A. iliyofulia, yule　　B. yule, kabisa
C. yaya, kabisa　　D. iliyofuliwa, kabisa

27. **Kamilisha nomino ya makundi .**
Charo cha________
A. wasafiri　　B. ng'ombe
C. miwa　　D. mahindi

28. Ni neno lipi lisilo katika ngeli moja na mengine?
A. Ndimi　　B. Mbao
C. Njuga　　D. Ndwele

29. <u>Ki</u> ya kielezi inapatikana katika sentensi ipi?
A. Kijiji kile hakina umeme
B. Kijanajali kina mazoea ya kuruka
C. Akifaulu tutashangilia
D. Yeye hupenda kusoma kimoyomoyo

30. **Jaza pengo kwa kiulizi mwafaka**
Mtabeba mizigo _______ ?
A. gani　　B. zipi
C. migani　　D. ngapi

**Soma kisa kifuatacho kwa makini kisha ujibu maswali 31- 40 kwa ufasaha**

Niliamka alfajiri na mapema kabla jua halijapenyeza jicho lake jekundu kutoka matlai. Nilipiga mswaki himahima na kuunawa uso wangu chapuchapu . Baada ya kujisukutua nilizivalia nguo zangu nadhifu nikapendeza na kuvutia kama ua la waridi. Hakika, ukiona vyaelea ujue vimeundwa.

Baada ya staftahi niliupachika mkoba wangu kwapani nikatoka nje. Nilipouacha mlango mgongoni ndipo nilipokumbuka kwamba sikuwa nimemuaga mama yangu mpenzi. Nilisikitika na kujilaumu kwamba nilikuwa na haraka isiyo baraka. Lakini nilielewa fika kuwa sahau ni hulka ya mja wala haina baraka. Niliubisha mlango naye ninangu akasema 'karibu' Nami nikaingia chumbani adabu mkononi, furaha usoni na shikamoo mdomoni.

"Marahaba mwanangu!" Mama alijibu, kwa pambaja na mapenzi halisi ya mama kwa mwanawe wa pekee. Mama alinikumbusha kuwasili kwa baba kutoka kazini . Baba yangu alikuwa akifanya kazi jijini Mwanza katika taifa jirani la Tanzania. Alipaswa kuwasili mjini Kisumu kwa meli ya jioni. Mimi na mama tulijiandaa rasmi kuenda kumlaki mwendo wa thenashara jioni hiyo. Nawapenda wazazi wangu si haba, kweli kipendacho roho ni dawa.

Naam, nilimuaga mama kwa furaha na bashasha isiyo kifani au kupimika ukipenda. Mchana kutwa nilikuwa na bashasha japo furaha zangu niliweza kuzibana ndani kwa ndani katika sakafu ya moyo wangu kama samaki bunju.

Darasani masomo yalikuwa rahisi bin mwewe .Si hisibati si somo la jamii, si kimombo , yote yalikuwa ya kupendeza. Maswali ya walimu nilikuwa wa kwanza kuyajibu tena kwa usahihi . Kila mja darasani alistaajabu kuwa najibu maswali huku bashasha ikionekana usoni mwangu.

Adhuhuri baada ya masomo ya asubuhi tulipanga foleni kuingia katika bwalo ili angalau tushtaki njaa na kufanyia chamcha chetu haki. Ugali kwa mboga ndicho chakula tulichoandaliwa . Chakula chenyewe kililika kiasi cha <u>**kunishibisha kama bweha mlafi**</u>. Kweli wahenga hawakufeli walipon<u></u>ena, njaa ni mwana malegeza na shibe ni mwana malevya.

Jioni ile nilipofika kiamboni mwetu, nilimpata mama amejitayarisha . Nami nikavalia mavazi ya kupendeza na sote tukaliabiri gari na mama kuelekea kwenye kituo cha meli kumlaki baba. Baada ya nusu saa, meli kutoka Mwanza ikawasili na tulifurahi ghaya kumwona baba. Alikuwa ametuletea zawadi chungu nzima. Mama wee ! Ilikuwa furaha isoyopimika.

Baba alichukua usukani na kuwa dereva , akatupeleka katika mkahawa mmoja kwa chajio chetu na tulikula mapochopocho ya kila nui.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

31. Ni kweli kudai kuwa mwandishi alikuwa amerauka mwendo wa saa______
A. moja unusu B. kumi na moja
C. mbili D. moja

32. Kwa nini methali , " ukiona vyaelea vimeundwa" imetumika katika aya ya kwanza ?
A. Jinsi ambavyo alichukua muda kuvaa
B. Ukiona jumba la kifahari ujue kazi nzito umefanywa na mtu fulani
C. Vinavyoelea ni vile vimeundwa
D. Mwandishi hajafafanua methali hii

33. Kwa mujibu wa aya ya tatu, mamake mwandishi ________
A. alimjulisha kuhusu ziara ya babake nyumbani asubuhi ile kwa mara ya kwanza
B. hakuwa na uhakika bwanake alikuwa aje nyumbani siku gani
C. alikuwa amemjulisha mwanawe kuwa babake alikuwa afike nyumbani siku ile, akamkubusha vile vile
D. alikuwa mgonjwa na ndio maana alikuwa katika chumba chake cha kulala

34. Babaye mwandishi alikuwa asafiri kwa _____
A. daladala B. ndege ulaya
C. meli D. gari moshi

35. Mwandishi alikuwa na furaha nyingi shuleni siku inayozungumziwa kwani
A. alikuwa na mazoea ya kufurahi sana
B. alikuwa anatamani kumuona babaye jioni ile
C. masomo yote shuleni yalipendeza
D. alikuwa amekula kiamsha kinywa kitamu na vilevile kula chamcha nzuri

36. Tunawezakudai kauli kuwa, mwandishi shuleni alikuwa
A. kichwa chepesi
B. kichwa maji
C. mtoto mkorofi
D mwanafunzi mdaku

37. Maneno **kunishibisha kama bweha mlafi** na yaliyopigiwa kistari yanaashiria nini?
A.Mwandishi kuwa mlafi ja bweha
B.Kuonyesha matumizi ya tashbihi
C. Kuonyesha jinsi alivyokuwa amekula chakula akashiba
D. Kuashiria jinsi chakula hakikulika vyema

38. Walipowasili kwenye kituo cha meli mwandishi na mamake walisubiri kwa muda gani ndiposa babake awasili ?
A. Mwandishi hajasema
B. Saa moja
C. Dakika thelathini
D. Sekunde thelathini

39. Babaye mwandishi alipowasili
A. alipeleka familia yake nyumbani mara moja
B. alitiririkwa na machozi ya furaha kuwaona watu wake
C. alikuwa mikono mitupu
D. aliwapeleka bibi yake na mwanawe kupata chakula cha jioni

40. Anwani inayofaa kisa ulichokisoma ni _____
A. Siku ya majonzi
B. Siku ya dhiki kuu
C. Siku ya bashasha
D. Ukiona vyaelea ujue vimeundwa

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50**

Alijulikana kwa jina Chaurembo. Kila mja shuleni pao alimfahamu vizuri sana japo alikuwa mwanafunzi mnyamavu, mpole na asiyependa vishindo. Mambo yake yalikuwa taratibu na yaliyoratibiwa, yakaratibika. Michezo mingi ya kubananga wakati na isiyo na maana hakuicheza. Ungempata ametulia tuli darasani akibukua, hasa wakati ya mgambo ilipokuwa imelia na wengi wakawa mbioni kufaya maandalizi **anuwai**.

Tangu hapo jadi alipokuwa katika madarasa ya chini, alikuwa miongoni mwa wale mabao walituzwa kila mwisho wa muhula kwa kutia fora katika mitihani ya darasa. Aliuthamini sana ushirikiano na wanafunzi wenziwe darasani, hasa wale waliokuwa na chudi za mchwa kama yeye. Mizozo ya kitoto darasani na wanafunzi waliopenda kulaza damu usingempata akijihusisha nayo kwani hakupenda kuumana meno na yeyote.

Alipohitimu darasa la saba na kujiunga na la nane aliendelea kuuma uzi ule ule . Bila shaka alimaizi kuwa atangaye sana na jua hujua Naam! Hakukosea miezi kadhaa ya papo kwa papo hatimaye jiwe ilikata kamba. Matokeo ya mtihani yalipotangwaza , la ibura lilitendeka . Kila mja hapo shuleni pao alijua kuwa banati Chaurembo angepita mtihani. Hata hivyo hakuna angefikiria kuwa angekuwa katika orodha ya wanafuzi mia moja bora katika taifa zima na jina lake kuchapishwa gazetini.

Alimiminiwa sifa mzomzo na kila mja, si walimu , si wazazi, si wakurugenzi na hata wanafunzi wenzake.Alipoitwa kujiunga na shule ya mabanati ya Starehe, ilikuwa ni fahari kubwa kwa kila mtu aliyehusishwa naye . Kuntu, achanikaye kwenye mpini ..............."

**41.** Chaurembo alikuwa na sifa zifuatazo ila?
A. Mpole
B. Asiyependa vishindo
C. Mnyamavu
D. Mwingi wa ajizi

**42.** Mambo ya Chaurembo yaliratibiwa yakaratibika sentensi imenyambuliwa katika hali ya
A. kutendeana
B . kutendeka
C. kutendesha
D. kutendatenda

**43.** Nini maana ya neno ***'anuwai'*** kama ilivyotumika
A. Maandalizi hasi
B. Maandalizi mengi
C. Maandalizi ya haraka
D. Maandalizi haba

**44.** Ungempata Chaurembo ametulia tuli kama maji ya mtungi . Huu ni mfano wa
A. tanakali za sauti
B. tashbihi
C. majazi
D. balagha

**45.** Ni kweli kusema kuwa katika madarasa ya chini Chaurembo __________
A. alikuwa Juha
B. alikuwa moto wa kuotea mbali
C. alikuwa kichwa maji
D. alilemewa sana kimasomo

**46.** Ni methali gani inaweza kujumlisha tabia za Chaurembo katika aya ya pili?
A. Fahali wawili hawakai zizi moja
B. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
C. Ujana ni moshi ukienda haurudi
D.Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti

**47.** 'Atangaye sana na jua hujua' ni kisawe cha
A. subira huvuta heri
B. mwenye pupa hadiriki kula tamu
C. mgagaa na upwa hali wali mkavu
D. mhini na mhiniwa njia yao ni moja

**48.** Jambo la ibura ni ________
A. jambo la lazima
B. jambo la kuhuzunisha
C. jambo la kuzingatiwa
D. jambo la kushangaza

**49.** " Wanagenzi waliokuwa na chudi kama yeye" imetumika kumaanisha ?
A. Waliolaza damu
B. Waliotia fora
C. Waliozembea masomoni
D. Waliokuwa na ajizi

**50.** "Achanikaye kwenye mpini ............" Alama ya uakifishaji iliyotumia ni ______
A. ritifaa
B. mlazo
C. koma
D. dukuduku